



# Tanzania yazidi kupenya kinyang'anyiro tuzo ITU

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WANANCHI wametakiwa kuipigia kura Tanzania ili iibuke mshindi katika tuzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayotolewa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa (ITU).

Tanzania imeingia katika kinyang'anyiro hicho baada ya mfumo wa eMrejesho kuchaguliwa kuwania tuzo hiyo ya kimataifa za WSIS 2025.

Hatua hiyo ni juhudi za kutambua miradi ya kibunifu duniani inayotumia TEHAMA kuchochea maendeleo kwa wananchi na taifa.

Mrejesho V2 imepenya hadi hatua ya mwisho ya mchujo katika kipengele cha e-Government (AL C7),kati ya zaidi ya maombi 1,000 yaliyowasilishwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Kwa mujibu wa Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Subira Kaswaga, taarifa ya kuchaguliwa kwa Tanzania kushiriki katika kinyang'anyiro hicho, ilipokelewa kupitia baruapepe kutoka ITU.

Subira, alisema ITU ilifafanua kuwa mfumo huo umetimiza vigezo vya kushindania tuzo hizo maarufu za TEHAMA duniani.

Mrejesho V2 ni jukwaa la kisasa lililoboreshwa kwa kutumia akili mnemba (AI) kukusanya, kuchambua na kuratibu mrejesho wa wananchi kuhusu huduma wanazopata kutoka taasisi za Serikali," alisema.

Alisema mfumo huo huwezesha wananchi kutoa maoni, mapendekezo na malalamiko kuhusu huduma wanazopokea na AI na kuchakatwa haraka.

**"Jukwaa hili litatuwezesha kupata uzoefu ambao Tanzania unao katika Utalii wa Vyakula kwani ina ardhi kubwa na hali ya hewa ni nzuri," alisema Grandcourt.**

Alisema hatma ya ushindi wa tuzo hiyo kwa Tanzania iko mikononi mwa wananchi kwa kupiga kura kwa wingi.

Subira, ameendelea kutoa wito kwa wananchi na na wadau wa TEHAMA duniani kuonyesha mshikamano kwa kupiga kura kabla ya Aprili 30, mwaka huu ili Tanzania iibuke kidedea

"Ili kupiga kura tembelea tovuti ya WSIS Prizes 2025 (https://www.itu.int/net4/wsis/stocktaking/Prizes/2025), tafuta AI Powered eMrejesho V2 kwenye kipengele cha e-Government (AL C7), na piga kura yako sasa ili tulete ushindi nyumbani,"alisema Subira na kusisitiza kuwa:

" Huu ni wakati wetu wa kupeperusha bendera ya taifa kimataifa na kuthibitisha kuwa ubunifu wa Kiafrika unaweza kushindana na dunia nzima."

Alisema washindi wa tuzo hiyo kwa mwaka huu, watatangazwa katika hafla itakayofanyika Jiji la Geneva nchini Uswisi kuanzia Julai 7 hadi 11, mwaka huu, wakati wa mkutano wa ngazi ya juu wa WSIS+20.

Mwaka jana, katika toleo la kwanza la mfumo wa eMrejesho, Tanzania liliibuka mshindi wa Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika huduma za umma kutokana na ubora na ubunifu wa kisekta wa taifa.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (katikati) akizungumza na waandishi wa habari na watumishi wa sekta ya madini jijini Dodoma jana, wakati akitoa taarifa ya kuongezeka kwa mchango wa pato la Taifa kwa kufikia asilimia 10.1 kwa mwaka 2024. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Msafiri Mbibo na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Yahya Samamba. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Makanisa yahimizwa waumini kuchangamkia Mei Mosi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

UMOJA wa Makanisa Mkoa wa Singida umewataka waumini mkoani hapa kuchangamkia fursa ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kitaifa kwa kufanya biashara ili kujiongezea kipato.

Mkuu wa Jimbo la Uaskofu Usharika wa Immanuel Singida Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati, John Kibuga, aliyasema hayo wakati wa ibada ya Jumatatu ya Pasaka iliyofanyika Viwanja vya Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Singida na kuhudhuriwa na waumini wa makanisa mbalimbali mkoani hapa.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan ambaye mwaka huu ametuona na kutuletea Mei Mosi mkoani Singida, hii ni fursa kama kanisa, ni fursa kama familia maana hapo tutafanya biashara kwa kuuza vyakula, tutakodisha viti, watu watasafirishwa kwenye vyombo vya moto," alisema.

Kibuga, alisema wageni watakaowasili Singida kwa ajili ya Mei Mosi, watambue kuwa ndio mkoa pekee Tanzania ambao kuku wa kienyeji na asali halisi vinapatikana.

Akizungumzia kuhusu Uchaguzi Mkuu utakaofanyika nchini Oktoba mwaka huu, alitaka haki itendeke kwa vyama vyote vya siasa na amani kudumishwa.

Aliwataka wananchi kutambua kuwa amani ni tunu kubwa katika taifa la Tanzania na haiwezi kuwepo kama hakuna haki, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuilinda iliyopo nchini.

Baadhi ya waumini waliishukuru Serikali ya Mkoa wa Singida kwa kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha kufanya biashara vizuri katika kipindi hiki cha kuelekea Mei Mosi.

## Madaktari bingwa wa Samia kupiga kambi Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MADAKTARI bingwa na bobezi wa Dk.Samia Suluhu Hassan wapatao 104 wataweka kambi kuanzia mwanzoni mwa wiki ijayo mkoani hapa kutoa matibabu kwa wananchi ya magonjwa mbalimbali.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, alisema madaktari hao watatoa huduma za matibabu hayo kwa awamu mbili.

Dengedo, alisema awamu ya kwanza itaanza jumatatu ijayo, Aprili 28 hadi Mei 3, mwaka huu kwa kuhusisha madaktari bingwa 49. Katika awamu hiyo, madaktari hao watatoa huduma kwa magonjwa ya watoto,uzazi na wanawake,upasuaji,huduma ya usingizi na ganzi.

Matibabu mengine ni ya magonjwa ya pua, koo, masikio, kinywa, meno na huduma ya uuguzi na kinga.

Madaktari hao, watatoa huduma hizo katika hospitali tembezi, ngazi ya halmashauri na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Awamu ya pili, itaanza Mei 5 hadi Mei 9, mwaka huu kwa kuhusisha madaktari bingwa na bobezi wapatao 55 katika fani 16.

"Katika zoezi hili la awamu ya pili tunatarajia kutoa huduma za kibingwa na mabingwa bobezi. Madaktari bingwa watatoka katika Hospitali za Rufaa za mikoa ya Dodoma,Morogoro,Pwani,Iringa wakishirikiana na wenyeji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida," alisema Dendego.

Alisema madaktari hao watatoa matibabu ya magonjwa ya ndani ya wanawake, uzazi, watoto, upasuaji wa mifupa, njia ya mkojo, masikio, pua, koo, urekebishaji wa kinywa, meno, radiologia, usingizi na ganzi.

Magonjwa mengine ni utengamao na viungo, mishipa ya fahamu na ubongo, ubungwa wa ngozi, afya ya akili na urekebishaji wa viungo. Ametoa wito kwa wananchi katika maeneo yao wazingatie ratiba ya utoaji huduma hizo kwa kufika katika hospitali za Halmashauri ili kuonana na madaktari hao na kupata matibabu.

"Tunamshukru Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea huduma hizi na hii ni fursa adhimu katika mkoa wetu, naomba wananchi waichangamkie ili waweze kupatiwa matibabu na madaktari bingwa hao, " alisisitiza.

CamScanner